**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UCHUKUZI**

**MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI**

# TAARIFA KWA WANAHABARI

# MAFANIKO YA LATRA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MINNE YA UONGOZI WA MHE. DKT SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA (AWAMU YA SITA)

*Dar es Salaam, 14 Aprili 2025*

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Shukrani

**Ndugu Wanahabari,** Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima, na fursa ya kukutana leo kwa lengo la kutoa taarifa kuhusu mafanikio ya utendaji wa LATRA katika kipindi cha miaka minne (4) ya Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na **Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**.

Pili, napenda kutumia fursa hii kutoa Pongezi za Dhati kwa **Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, kwa Uongozi wake mahiri wa Serikali ya awamu ya sita wenye mafanikio mengi makubwa. Kwa maneno uchache, niseme tu kwamba, **Uongozi wa Mhe. Rais, Dkt Samia Suluhu Hassan umetujengea mazingira rafiki yenye ushirikishaji wa wadau katika kusimamia sekta ya usafiri ardhini**. Ninawapongeza pia uongozi mahiri na madhubuti wa wasaidizi wake, wakiwemo **Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi, Mhe. David Kihenzile (Mb), Naibu Waziri wa Uchukuzi, Prof. Godius W. Kahyarara, Katibu Mkuu - Wizara ya Uchukuzi,** pamoja na **Mha. Ludovick Nduhiye, Naibu Katibu Mkuu - Wizara ya Uchukuzi.**

Tatu, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru sana **watoa huduma** zinazodhibitiwa na LATRA, **watumiaji wa huduma** za usafiri ardhini, pamoja na **wadau wetu wote**, zikiwemo taasisi za umma na sekta binafsi kwa ushirikiano waliotupatia katika katika kipindi chote cha utendaji wetu. LATRA imepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa wadau wetu mmoja mmoja na kupitia vyama vyao ikijumuisha TABOA, TAT, TATOA,

TAMSTOA, TRFA, AKIBOA, KIBOA, DARCOBOA, UWADAR, KIBABOT na vinginevyo. Tunaahidi kuuenzi ushirikiano uliopo katika kutekeleza majukumu yetu kwa weledi, na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu zilizopo.

Mwisho, sio kwa umuhimu, niwashukuru sana ninyi Wanahabari pamoja na Wamiliki wa Vituo na Vyombo vya Habari kwa kutumia vyema taaluma zenu katika kuuhabarisha na kuuelimisha umma. Wino wa Kalamu zenu zina thamani kubwa sana katika kujenga Taifa lenye umoja, mshikamano, utulivu na amani ya kudumu. Asanteni sana na LATRA tutaendelea kuwathamini na kuthamini kazi zenu.

## 1.2 Kuanzishwa kwa LATRA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ilianzishwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura 413 ili kudhibiti huduma za usafiri kwa njia ya Reli, Barabara na Waya; ikipokea majukumu haya kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA). LATRA ilianza kazi rasmi mnamo tarehe 29 Aprili, 2019 baada ya Sheria yake kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 358 la tarehe 26 Aprili, 2019.

## 1.3 Ofisi za LATRA

LATRA ina **ofisi katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara**. Aidha, katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Sita, LATRA imesogeza huduma zake karibu zaidi na wananchi kwa kufungua ofisi katika maeneo ya kimkakati kwenye baadhi Halmashari za miji na wilaya nchini, ambapo tayari **tumefungua ofisi kumi (10).** Maeneo hayo ni Kituo cha Mabasi cha **Magufuli - Mbezi, Tegeta, na Mbagala (Dar es Salaam).** Maeneo mengine ni **Makambako (Njombe), Kahama (Shinyanga), Masasi (Mtwara), Ifakara (Morogoro), Korogwe (Tanga), Same (Kilimanjaro), na Nzega (Tabora).** Hatua hii ni sehemu ya mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita.

Katika kuendelea na juhudi za kusogeza huduma za LATRA karibu na wananchi, taratibu za kuanzisha Ofisi zingine **tano (5)** zinaendelea katika maeneo ya **Gongo la Mboto (Dar es Salaam), Mkuranga (Pwani), Chunya (Mbeya), Mufindi (Iringa),** na **Nyakanazi (Kagera).**

## 2.0 DIRA, DHAMIRA NA MISINGI MIKUU

**Ndugu Wanahabari,** Pamoja na kuongozwa na misingi ya Sheria, LATRA inazingatia **Dira (Vision), Dhamira (Mission) na Misingi Mikuu (Core Values)** iliyojiwekea na kuifuata kwenye utendaji kazi na majukumu ya kila siku.

***a) Dira:*** Nchi yenye huduma za Usafiri Ardhini zenye *usalama, uhakika* na *rafiki wa mazingira*.

***b) Dhamira:*** Kusimamia huduma za Usafiri Ardhini kwa *kutoa leseni*, *ufuatiliaji* na *ukuzaji wa ushindani* kwa ajili ya ustawi wa Tanzania.

***c) Misingi Mikuu***

| | |
|---|---|
| i) **Weledi:** | Tunaonesha maarifa, ujuzi na mtazamo chanya kwenye kazi zetu; |
| ii) **Uwajibikaji:** | Tunajitahidi kubeba dhamana ya utendaji wetu; |
| iii) **Kufanya kazi kwa pamoja:** | Tunafanya kazi kwa pamoja ili kufikia malengo yetu tuliyojiwekea; |
| iv) **Uadilifu:** | Tuna uaminifu na uadilifu katika kuwahudumia wadau wetu |
| v) **Uwazi:** | Tunatekeleza majukumu yetu kwa uwazi na kwa ushirikiano; na |
| vi) **Ubunifu:** | Tunajitahidi kutafuta njia bora za kuongeza thamani ya huduma zetu |

## 3.0 MAFANIKIO KATIKA MIAKA MINNE YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

**Ndugu Wanahabari,** Mafanikio ya LATRA katika kipindi cha miaka minne (04) ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** kuanzia Mwezi Februari, 2021 hadi Mwezi Machi 2025 ni kama ifuatavyo: -

### 4.1 Udhibiti Usafiri wa Barabara

#### 4.1.1 Utoaji Leseni kwa Vyombo vya Usafiri kwa Njia ya Barabara

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)( b) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413, LATRA ina wajibu wa **kutoa, kuhuisha, kusitisha na/au kufuta leseni za usafirishaji**. Idadi ya leseni za usafirishaji zilizotolewa kwa vyombo vya usafiri wa abiria (passenger service vehicles), mizigo (goods carrying vehicles), na vyombo vya usafiri wa kukodi (private hire service vehicles) ziliongezeka kutoka **226,201** mwaka

**2020/21** (Februari, 2021) hadi **334,859** mwaka **2024/25** (Machi, 2025), ikiwa ni ongezeko la leseni **108,658,** sawa na ongezeko la **asilimia 48.** Hili ongezeko ni sawa na wastani wa ongezeko la asilimia 12 kila mwaka katika kipindi cha miaka minne (4).

### 4.1.2 Kufikisha Huduma Karibu na Wananchi

LATRA imefungua ofisi ndogo kumi (10) kwenye maeneo mbalimbali ya kimkakati na hivyo kuwa na jumla ya Ofisi 37 nchi nzima. Kufikia mwezi Machi 2025, ofisi hizi ndogo zimeonesha mafanikio katika kufikia wananchi walio mbali na miji mikuu ya mikoa, kuboresha udhibiti wa bodaboda, kutatua migogoro ya wadau katika maeneo hayo, kufikisha elimu kwa wadau na kusogeza ushirikiano na mamlaka mbalimbali kwenye maeneo hayo, ikiwemo Serikali za Mitaa (LGAs), Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) na mamlaka zingine zilizopo kwenye maeneo hayo.

### 4.1.3 Maboresho ya Usafiri wa Mabasi ya Mijini

LATRA imeendelea kuboresha usafiri wa umma katika miji na majiji makubwa hapa nchini. **LATRA imeanzisha njia mpya 1,007 za daladala Mkoani Dar es Salaam** ili kufika maeneo yasiyofikika na kurefusha baadhi ya njia kwa lengo la kumpunguzia gharama mwananchi. Njia za usafiri wa mabasi ya mijini zilizorefushwa ni kama ifuatavyo:

**a) Dar es Salaam:**

i) **Mbezi Luis – Kisarawe** kupitia barabara ya **Malamba Mawili, Ban**ana
ii) **Toangoma – Pugu Stesheni** kupitia barabara ya **Kilwa, Nyerere**
iii) **Kivukoni - Bunju Sokoni** kupitia Barabara ya **Bagamoyo**,
iv) **Gerezani - Bunju Sokoni** kupitia Barabara ya **Bagamoyo**,
v) **Buyuni Sokoni - Stendi Kuu ya Magufuli** kupitia **Kinyerezi**
vi) **Bunju Sokoni - Stendi Kuu ya Magufuli** kupitia **Madale**
vii) **Mbande Kisewe - Gerezani** kupitia Barabara ya **Kilungule, Chang'ombe, Usalama**,
viii) **Mvuti - Machinga Complex** na **Tabata Segerea**,
ix) **Ngobedi B -Machinga Complex** kupitia **Nyota Njema**, na
x) **Kitonga - Gerezani** kupitia barabara ya **Kilwa**.

**b) Arusha:**

LATRA imefanya mabadiliko ya njia za daladala kwa kuzifanya baadhi ya njia kuwa za mzunguko kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa huduma kwenye baadhi ya maeneo ambayo hayakuwa na huduma. Mfano ni njia inayoanzia **Kwa Mrombo kupitia Impala, Philips, Sanawari, Chuo cha Ufundi Arusha hadi 'Fire' na kurudi kwa Mrombo**.

**c) Dodoma**

Katika Jiji la Dodoma, Makao Makuu ya nchi, zimeanzishwa njia mpya kwa ajili ya kuyafikia maeneo mapya ya makazi mapya kutokana na kukua kwa kasi kwa Jiji la Dodoma. Mfano wa njia hizo ni:

i) **Machinga Complex - Njedengwa,**
ii) **Machinga Complex - Mpamaa,**
iii) **Machinga Complex - Chidachi**,
iv) **Machinga Complex - Nzuguni**,
v) **Machinga Complex – Swaswa, na**
vi) **Vyeyula - Ilazo**.

Hatua ya kuhamishia daladala kituo cha Machinga Complex kumesaidia kuwepo kwa njia za mzunguko katikati ya Jiji la Dodoma na hivyo kuongeza upatikanaji wa huduma kwa wananchi. Mzunguko huo ni kuanzia barabara ya **Hospitali kupitia Majengo Sokoni hadi Machinga Complex** kisha kupitia **Uwanja wa Ndege** na kurudi mjini.

**d) Jijini Mwanza**

Katika Jiji la Mwanza, zimeanzishwa njia ndefu kwa ajili ya kuyafikia maeneo mapya ya makazi na kukua kwa kasi kwa Jiji la Mwanza. Mfano wa njia hizo ni kutoka:

i) **Usagara – Kisesa kupitia Buzuruga;**
ii) **Ilalila – Misungwi kupitia Buzuruga;**
iii) **Nyashishi – TX kupitia Kiseke - PPF;**
iv) **Nyashishi – Kisesa Kona ya Kayenze kupitia Mecco**
v) **Nyashishi – Ilalila kupitia Buzuruga;**
vi) **Mwanza mjini – Igombe**
vii) **Mwaloni – Kona ya Kayenze; na**
viii) **Mwaloni – Kabusungu.**

#### 4.1.4 Uthibitishaji wa Madereva

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)(e) cha Sheria ya LATRA Sura 413, LATRA ina jukumu la kusajili wahudumu na kuthibitisha madereva wa vyombo vya usafirishji vinavyodhibitiwa. Lengo la kuthibitisha madereva ni kuwa na madereva wenye weledi wa kuendesha magari yanayotoa huduma za usafiri wa umma na mizigo kwa usalama.

Mamlaka imekuwa ikiwasajili madereva na baadae kuwapatia vyeti vya kuthibitishwa baada ya kufaulu **mtihani wa kuthibitishwa inayofanyika katika Ofisi za LATRA za Mikoa yote 26 Tanzania Bara**. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2025, **madereva 33,778** walikuwa wamesajiliwa na taarifa zao kuingizwa kwenye Kanzidata (Database) ya Mamlaka. Kati ya madereva hawa, **madereva 8,172** wamesajiliwa kwenye Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Mabasi (VTS) na kupatiwa Kitufe cha Utambuzi wa Dereva (i-button), na **madereva 4,563** walifaulu mitihani ya LATRA kati ya **9,191 waliofanya mitihani** huo (sawa na ufaulu wa **asilimia 49.65**) na kupatiwa vyeti vya kuthibitishwa. Matokeo haya yanaashiria **maandalizi hafifu kwa madereva, woga wa mitihani unaofanywa kwa kompyuta, upya wa zoezi la kuthibitisha madereva, na kukosekana kwa utaratibu wa kujisomea/kujiendeleza kwa madereva**.

Muhtasari wa taarifa za madereva waliofanya mitihani na kufaulu/kuthibitishwa katika kipindi cha 2022/23 (Novemba, 2023) hadi 2024/25 (Machi, 2025) ni yameoneshwa kwenye Jedwali Na 01:

**Jedwali Na. 01: Idadi ya Madereva Waliothibitishwa na LATRA**

| 2022/23 | | | 2023/24 | | | 2024/25 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Waliofanya Mtihani | Waliofaulu na Kuthibitishwa (Idadi) | % | Waliofanya Mtihani | Waliofaulu na Kuthibitishwa (Idadi) | % | Waliofanya Mtihani | Waliofaulu na Kuthibitishwa (Idadi) | % |
| 1,707 | 1,061 | 62 | 3,879 | 1,952 | 50 | 3,605 | 1,550 | 43 |

***Chanzo:*** *LATRA (2025)*

#### 4.1.5 Usimamizi wa Usafiri wa Mabasi Usiku na Mchana (24/7)

Serikali ya Awamu ya Sita iliondoa zuio la mabasi ya abiria kusafiri nyakati za usiku lililowekwa mwaka 1994. Akitoa Hoja ya kuahirisha Mkutano wa 11 wa Bunge la Bajeti tarehe 28 Juni, 2023, **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** aliziagiza, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Uchukuzi kuweka utaratibu mzuri wa usimamizi wa mabasi nyakati za

usiku. LATRA ilishiriki katika zoezi la kufanya maandalizi ya kuanza kwa safari za usiku kwa kushirikiana na wadau wake muhimu, hasa wamiliki wa mabasi (wakiwemo TABOA) na ilitekeleza maamuzi ya Serikali kwa kuanza kutoa ratiba za mabasi kusafiri usiku na mchana (24/7) kuanzia tarehe **1 Oktoba, 2023**.

Tarehe 29 Septemba, 2023, akitangaza kwa niaba ya Serikali kuanza kwa ratiba za safari za usiku, aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Jumanne Sagini (Mb), alieleza sababu sita (06) za Serikali kuruhusu safari za usiku kama ifuatavyo *(**Ninanukuu**):*

i) *Udhibiti wa usalama kupitia Jeshi la Polisi umeimarishwa kutokana na jitihada za Serikali ya Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;*
ii) *Mwamko wa wananchi, hususan wafanyabiashara kutumia taasisi za kifedha badala ya kusafiri na fedha taslimu (cash) umeongezeka;*
iii) *Serikali imeimarisha huduma za mawasiliano ya simu kwa kujenga minara ya mawasiliano kwenye maoneo mengi Nchini;*
iv) *Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inao Mfumo madhubuti wa Kufuatilia Mwenendo wa Mabasi (VTS) unaofanyakazi kwa saa 24;*
v) *Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi imeboresha miundombinu ya usafiri, hususan barabara kuu na barabara za mikoa na hivyo kufanya Nchi yetu kuwa moja ya Nchi zenye usafiri wa barabara unaoaminika na bora; na*
vi) *Wafanyabiashara wengi wanaomiliki mabasi ya abiria walio tayari kufanya safari za saa 24 wako tayari pia kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo kuhusu usafiri na usafirishaji wa abiria.*

*(**Mwisho wa Kunukuu**).*

**Ndugu Wanahabari,** Tangu kuanza kwa huduma za usafiri wa 24/7, LATRA imeendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi, Kikosi cha Usalama Barabarani katika uratibu wa huduma za usafiri wa mabasi kwa kuimarisha usimamizi wa masharti ya leseni ikiwemo **ukaguzi wa mabasi, utambuzi wa madereva kwa *i-buttons* na kongeza matumizi ya VTS**. Hadi kufikia tarehe **31 Machi 2025, mabasi 2,323 yalikuwa yamepatiwa ratiba za kutoa huduma za usafiri usiku na mchana (24/7)**.

Aidha, tathmini ya LATRA ya mwaka mmoja wa utekelezaji wa ruhusa hii ya safari za usiku na mchana (24/7) umeonesha **Wananchi wengi wamefurahishwa na kuridhishwa na maamuzi ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan** kuondoa zuio la mabasi kusafiri usiku. Aidha, kuna **mwitikio mkubwa wa Wananchi kutumia usafiri wa usiku kuliko mchana,** na **msongamano wa abiria kwenye Stendi umepungua sana, na 'mchezo' wa mabasi kukimbizana umepungua sana na unaelekea kwisha kabisa**. Vilevile, tathmini ya LATRA inaonesha kuwa **safari hizi za 24/7 zimepunguza gharama za njiani kwa abiria na kuboresha matumizi ya muda wao kwenye shughuli za kiuchumi, kijamii na kujiongezea vipato**.

### 4.2 Udhibiti Usafiri wa Reli

#### 4.2.1 Udhibiti wa Usalama wa Huduma za Reli

**Ndugu Wanahabari,** Usafirishaji kwa njia ya reli nchini ni mojawapo ya eneo linalodhibitiwa na LATRA kwenye maeneo ya **usalama wa miundombinu na mabehewa, nauli, viwango vya ubora na ufanisi wa utendaji**. Katika hatua ya kutimiza majukumu haya, LATRA katika kipindi kinachoanzia Februari, 2021 hadi Machi, 2025 **imefanya jumla ya kaguzi 275 katika miundombunu, ishara na mawasiliano**, **vitembea reli** (vichwa na mabehewa) **na uendeshaji.** Kati ya kaguzi hizi, **143 zilikuwa kwa Shirika la Reli Tanzania (TRC), na kaguzi 132 zilikuwa kwa Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)**.

#### 4.2.2 Uanzishwaji wa Huduma za Treni za SGR

**Ndugu Wanahabari,** katika maandalizi ya kuanza kwa huduma za usafiri wa abiria kwa treni za SGR, LATRA ilikuwa na jukumu la **kuthibitisha ubora wa vitembeareli** kabla ya kuanza kutoa huduma. LATRA iliungana na timu ya wataalamu wa TRC na Wizara ya Uchukuzi kwenda Nje ya Nchi (zilikokuwa zinaundwa) na **kukagua na kuthibitisha. Jumla ya vichwa vya treni 17**, **Mabehewa ya abiria 56**, **treni za seti za umeme (EMU) 10** na **Mabehewa ya mizigo 264** yamekaguliwa kipindi cha uundwaji katika nchi za **Korea, China, Malaysia na Ujerumani**. Pia Mamlaka imefanya **kaguzi za majaribio kwa mabehewa na vichwa** hivyo baada ya kuwasili nchini **kabla ya kuanza kutumika kutoa huduma**.

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, LATRA ilitekeleza jukumu la kisheria chini ya Kifungu cha 5(1)(c) kwa kupanga nauli za daraja la uchumi (Economy Class) wakati wa uanzishwaji wa huduma za treni ya kisasa (SGR). Kwa mujibu wa kifungu cha 19 cha Sheria ya LATRA, Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA iliidhinisha nauli za abiria kwa daraja la uchumi (economy class) kwa treni inayosimama kila kituo na treni inayosimama vituo maalum (express train) na kuanza kutumika mwezi Juni 2024.

**Nauli za Treni ya SGR zilitangazwa kwa Taarifa ya Kawaida Na 8931 kwenye Gazeti la Serikali Toleo Na 24 la 14 Juni 2024** zikiwa ni Shilingi 31,000 kwa treni ya kawaida (inayosimama kila kituo) na Shilingi 50,000 kwa treni inayosimama vituo maalum (express) kati ya Dar-es-Salaam na Dodoma. Nauli zilizoidhinishwa zimeelekeza mtoto mwenye umri kuanzia miaka minne hadi miaka 12 kutozwa nusu ya nauli na mtoto mwenye umri chini ya miaka minne kutotozwa nauli. Aidha, **LATRA iliruhusu TRC kujipangia nauli za SGR kwa Daraja la Biashara (Business Class) na madaraja mengine ya juu (Royal Class)** kwa kuwa eneo hili ni kwa abiria wenye uwezo kifedha na wanaoweza kufikia huduma hii.

### 4.3 Udhibiti Usafiri wa Waya (Cable Transport Regulation)

**Ndugu Wanahabari,** Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa (2021/2022 hadi 2025/2026) imeelekeza maboresho katika huduma za utalii nchini. Katika kutekeleza jukumu hili, LATRA imefanya utambuzi wa mahitaji, utayari wa wadau, na maeneo ya uwekezaji nchini. **Tathmini ya awali ya LATRA** imebainisha maeneo yenye vivutio yaliyopo kwenye mikoa nane (08) ya **Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Iringa, na Mbeya.** Aidha, rasimu ya Kanuni za Udhibiti wa Usafiri wa Waya zilishaandaliwa na Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikisha wadau. Kanuni hizo zilijadiliwa kwenye kikao cha Wadau kilichofanyika tarehe 23 Disemba 2024. Pia, Bodi ya LATRA kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina, Wizara ya Uchukuzi, na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inakamilisha mapitio ya Muundo wa Uongozi na Mgawanyo wa Majukumu ili kuunda Kitengo cha Udhibiti Usafiri wa Waya na kuwezesha usimamizi wa Kanuni za Usafiri wa waya, pindi zitakapokamilika na kuidhinishwa na Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi kwa mujibu wa Kanuni ya 45 ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413.

## 4.4 Kukuza matumizi ya TEHAMA kwenye utoaji wa huduma

### 4.4.1 Mfumo wa Usimamizi wa Shughuli za Kiudhibiti (RRIMS)

**Ndugu Wanahabari,** LATRA inazingatia ubunifu na haswa matumizi ya TEHAMA katika utendaji wa kazi. Katika kipindi hiki, LATRA imejenga mfumo wa TEHAMA unaojulikana kama Railway and Road Information Management System (RRIMS) ambao ni mfumo mkuu wa utoaji leseni, usajili madereva, malipo na taarifa za udhibiti. Mfumo wa RRIMS umeunganishwa na mifumo ya taasisi nyingine za serikali kama vile TRA, TIRA, NIDA, GePG na BRELA ili kurahisisha uhakiki. Kadhalika, Mfumo huu unamwezesha msafirishaji kufanya maombi ya leseni na huduma zake pamoja na kuchapa leseni iliyoidhinishwa ndani ya saa 24 bila uhitaji wa kufika ofisi za LATRA, na hivyo kupunguza kwa kiwango kikubwa usumbufu na muda wa kupata huduma.

### 4.4.2 Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS)

**Ndugu Wanahabari,** LATRA ilianzisha Mfumo wa Kufuatilia mwenendo wa Magari (Vehicle Tracking System – VTS) unaotumia 'Satelite', Kifaa cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTD), Mtandao wa Mawasiliano na Vifaa vya Uhifadhi Data Taarifa (GPS Data Servers) vinavyofanya kazi kwa pamoja ili kutuma taarifa za mwenendo mzima wa safari za chombo husika. Mfumo huu unalenga kusimamia matakwa ya usalama wa huduma kama ilivyoelekezwa kwenye Kifungu cha 5(1)(d) na Kifungu cha 6(g) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413, LATRA.

Mafanikio ya usimamizi wa magari kwa mfumo huu kufikia Machi 2025 yanaonekana kama ifuatavyo:

(a) Jumla ya magari **11,826** yalikuwa yameunganishwa kwenye mfumo.

(b) Kati ya hayo, magari **8,969** yanayotuma taarifa kwenye mfumo mpaka sasa.

(c) Wastani wa magari **5,800** yanafanya safari kila siku katika nchi yetu. Idadi hiyo huongezeka katika kipindi cha mwisho wa mwaka na hufikia mpaka magari **6,200** yanayofanya safari kwa siku.

(d) Katika magari yasiyotuma taarifa, baadhi hayapo barabarani kutokana na sababu mbalimbali kama
   - (i) Matengenezo ya muda mrefu.
   - (ii) Ajali
   - (iii) Kuungua moto
   - (iv) Baadhi yamebadili njia (route) na kuhamia kwenye njia ambazo hazina uhitaji wa kufunga vidhibiti mwendo (VTS)

**Jedwali Na. 02: Idadi ya magari yaliyounganishwa VTS**

| S/n | Mwaka wa Fedha | Idadi ya Magari Yote |
|---|---|---|
| 1 | 2021/2022 | 5,979 |
| 2 | 2022/2023 | 7,626 |
| 3 | 2023/2024 | 9,951 |
| 4 | 2024/2025 | 11,836 |

***Chanzo:*** *LATRA (2025)*

Aidha, Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) umewezesha utambuzi wa madereva aliyethibitishwa, wakati akiwa barabarani. Idadi ya madereva waliopewa vitufe vya utambuzi (i-Button) inaoneshwa kwenye Jedwali Na. 03.

**Jedwali Na. 03: Vitufe vya Utambuzi (i-button) wlizopewa madereva**

| S/N | Mwaka wa Fedha | Vitufe Vilivyogawiwa kwa Madereva |
|---|---|---|
| 1 | 2022/2023 | 256 |
| 2 | 2023/2024 | 1,797 |
| 3 | 2024/2025 | 6,119 |

***Chanzo:*** *LATRA (2025)*

### 4.4.3 Mfumo Jumuishi wa Utoaji Tiketi (CeTS) – Safari Tiketi

**Ndugu Wanahabari,** LATRA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA), Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA) pamoja na wadau wengine tumeunda mfumo jumuishi ulioounganishwa na mifumo mingine ya utoaji tiketi ukiwemo wa TRC na mifumo ya tiketi za mabasi ili kurahisisha ukataji tiketi na kutunza taarifa za abiria.

Katika kutekeleza Mfumo huu (CeTS) ambao unaweka **Stendi za Mabasi na Treni Kiganjani**, LATRA kwa kushirikiana na **Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA), Shirika la Reli Tanzania (TRC), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), na Watoa Huduma wa Tiketi za Kielektroniki** (e-Ticketing Vendors), **imekamilisha kuunganisha Mifumo ya e-Ticketing ya TRC (MGR,… SGR inaendelea),** pia **imeunganisha mifumo ya e-Ticketing Vendors 13, na wengine wawili (02) wanaendelea na taratibu za kuunganishwa kwenye CeTS.**

Hivyo, tangu kuanza kuunganisha mifumo ya Ticketi za Kielektroniki kwenye CeTS, tarehe 02/08/2024 hadi tarehe 31/03/2025, taarifa zetu zinaonesha **jumla ya abiria (miamala ya tiketi za kielektroniki) 13,429,549 ilifanyika kwenye CeTS.** Idadi hii ni sawa na wastani wa **abiria (miamala) 58,137 zinaonekana kwa siku**, sawa na wastani wa **abiria (miamala) 1,744,100 kwa mwezi** katika kipindi hicho cha **siku 231**, takriban miezi nane tangu kuanza kutumia mfumo huu.

Hivyo, Mfumo huu (CeTS) utakapotekelezwa ipasavyo, itaboresha sana huduma za usafiri wa umma kwa wananchi/abiria kupata tiketi zao kutoka kwenye dirisha moja na kujichagulia usafiri wa daraja analomudu na kwa njia anayokwenda. Aidha, Mfumo huu utawapa wamiliki taarifa sahihi za miamala yao, na kwa Serikali, itasaidia katika kuweka mipango ya kuboresha usafiri huu ikiwa ni pamoja na mipango ya ruti. Mfumo huu ukikamilika vyema kwenye usafiri wa mabasi ya mikoani na Nchi jirani, utaelekezwa kwenye mabasi ya mijini (daladala) na usafiri wa kukodi.

### 4.4.4 Mfumo Tumizi wa LATRA (LATRA App)

**Ndugu Wanahabari,** LATRA imeandaa mfumo tumizi unaopatikana kwenye simujanja 'Play Store' za aina ya *Android*. Huduma hii inamwezesha mwananchi kupata taarifa za nauli za mabasi, kutambua uhalali wa leseni za magari na adhabu, hivyo kumuwezesha abiria kuepuka kutumia gari lenye changamoto ili kujiepusha na usumbufu.

### 4.4.5 Matumizi ya Mfumo wa e-Mrejesho

**Ndugu Wanahabari,** LATRA inatumia Mfumo wa Serikali wa e-Mrejesho unaotumika kwa ajili ya kupokea Malalamiko, Mapendekezo, Pongezi au Maulizo. Mfumo unapatikana kwa anwani ya emrejesho.gov.go.tz au kwa kupakua mfumo tumizi wa e-Mrejesho au kwa kutumia simu kwa njia ya msimbo (USSD) au kwa kupitia tovuti ya LATRA www.latra.go.tz sehemu ya tovuti mashuhuri. Hivyo, tunawasihi wananchi wote kutumia mfumo huo na tunawahakikishia kushughulikia masuala yatakayowasilishwa ndani ya siku 21 tangu utakapowasilisha lalamiko au maulizo yako.

### 4.5 Elimu kwa Umma na Maonesho

#### 4.5.1 Uandaaji na Urushaji wa Vipindi vya Elimu kwa Umma

**Ndugu Wanahabari,** LATRA kupitia studio yake iliyoko Dar es salaam imeendelea kuandaa maudhui na vipindi vya elimu kwa umma; na kuvirusha kupitia Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC1), Clouds TV na mitandao ya kijamii kama vile 'LATRA Online TV' (You tube, Instagram, Facebook na X). Aidha, katika kipindi cha miaka minne ya taarifa hii, LATRA iliandaa na kurusha **vipindi 365**, vikiongezeka kila mwaka haswa kupitia mitandao ya kijamii. Jedwali Na 04 linaonesha taarifa ya vipindi vilivyoandaliwa na kurushwa katika kipindi cha 2020/2021 hadi 2023/2024.


**Jedwali Na 04: Vipindi vya Televisheni na Mitandao ya Kijamii, 2020/21-2023/24**

| Na. | Aina ya Vipindi | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vipindi vya Runinga (TV) | 40 | 48 | 52 | 52 | **192** |
| 2 | Mitandao ya Kijamii | 12 | 30 | 63 | 68 | **173** |
| | **Jumla** | **52** | **78** | **115** | **120** | **365** |

***Chanzo:*** *LATRA (2025)*

Aidha, kuanzia **Julai, 2024 hadi Machi, 2025** jumla ya **vipindi 113** viliandaliwa na kurushwa kwenye Runinga na Mitandao ya Kijamii ili kuelimisha umma kuhusu masuala mbalimbali ya kiudhibiti yanayotekelezwa na LATRA. Kielelezo Na. 01 hapa chini kinaonesha vipindi vilivyorushwa kupitia Televisheni na Mitandao ya Kijamii katika kipindi cha 2020/2021 hadi 2023/2024.

**Kielelezo Na 1: Vipindi vya Televisheni na Mitandao ya Kijamii, 2020/21 – 2023/24**




***Chanzo:*** *LATRA*

#### 4.5.2 Ushiriki katika Maonesho na Tuzo

**Ndugu Wanahabari,** LATRA imeendelea kushiriki kwenye maonesho mbalimbali ya Kitaifa na Kisekta kwa lengo la kutoa elimu kwa wananchi, yakiwemo maonesho ya **Sabasaba**, **Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani Tanzania Bara**, **Maonesho ya Nanenane**, **Wiki ya Usalama Barabarani Zanzibar**, **Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma** na **Mkutano wa Mwaka wa Sekta ya Uchukuzi**. Katika kipindi cha miaka miwili mfululizo, LATRA imetambulika kwa jitihada za kutoa elimu kwa umma na kupewa tuzo mbalimbali katika maonesho haya.

#### 4.5.3 Huduma kwa Wateja

**Ndugu Wanahabari,** LATRA imeanzisha kituo cha huduma kwa wateja mwaka 2023/24 kinachofanya kazi kwa saa zote ili kurahisisha utatuzi wa migogoro na changamoto kwa wakati. Huduma za kituo hicho zinapatikana kupitia namba za kupiga bila malipo **0800110019** na **0800110020**. Aidha LATRA imeendelea kuzitangaza namba hizi kupitia vipindi vya elimu kwa umma, mitandao ya kijamii na kuzibandika katika maeneo mbalimbali yanayofikiwa na wadau wetu. Kwa sasa, namba hizi zinaandikwa kwenye milango ya mabasi ya mijini sambamba na viwango vya nauli. Tathimini ya wateja ya mwaka 2023/2024 inaonesha asilimia 82 ya wateja wanaridhika na huduma za msingi za LATRA.

### 4.6 Utatuzi wa Migogoro

**Ndugu Wanahabari,** Utatuzi wa migogoro ni moja ya kazi za LATRA inayoelekezwa na Kifungu cha 5(1)(h) cha Sheria ya LATRA Sura ya 413. LATRA hupokea na kushughulikia migogoro baina ya watoa huduma, watoa na watumiaji huduma, na baina ya watumiaji huduma. Muelekeo wa malalamiko katika miaka mitatu iliyopita unaonyesha ongezeko la mwamko wa watumiaji huduma kuwasilisha malalamiko, huku kiwango cha utatuzi kikiwa cha zaidi ya asilimia 90 kila mwaka; ikiashiria uweledi katika kushughulikia migogoro kama inavyoonekana katika jedwali Na. 05 hapo chini.

**Jedwali Na 05: Utatuzi wa Malalamiko yaliyopokelewa kati ya 2022/23 – 2024/25**

| Mwaka wa Fedha | Malalamiko Yaliyopokelewa | Malalamiko Yaliyotatuliwa | Malalamiko Yaliyokatiwa Rufaa | Malalamiko Yaliyobaki | % Yaliyo tatuliwa |
|---|---|---|---|---|---|
| **2022/23** | 234 | 234 | 0 | 0 | **100.0%** |
| **2023/24** | 286 | 258 | 21 | 7 | **90.2%** |
| **2024/25** | 287 | 265 | 2 | 20 | **92.3%** |

*Chanzo: LATRA*

## 4.0 HITIMISHO

Kwa mwaka huu wa fedha 2024/2025 LATRA imejipanga kuhakikisha kuwa huduma za usafiri ardhini kwa abiria, mizigo na wa kukodi zinakuwa bora na salama zaidi, zinawafikia wananchi, kuondoa kero na changamoto mbalimbali katika sekta. Hii ni katika kutafsiri **maono** na kutekeleza **maelekezo** ya **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** katika kuwatumikia Watanzania na kufikia matarajio yake na ya Serikali nayoiongoza.

Aidha, LATRA imejipanga kusimamia huduma za usafiri ardhini ambapo huduma za usafiri wa barabara na reli zina mchango mkubwa katika kukuza uchumi na kuwezesha Tanzania kufanya biashara na Nchi za Jumuia ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na nchi za Jumuia ya Afrika Mashariki (EAC).

Ninapoelekea kumalizia mazungumzo yangu, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru tena Wanahabari wote mliopo hapa kutoka vyombo mbalimbali vya habari (magazeti, radio, televisheni na mitandao ya kijamii) na wengine popote walipo, kwa ushirikiano mzuri mliotupatia na mnaoendelea kutupatia hasa katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt Samia Suluhu Hassam, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuufikishia umma habari mbalimbali zikiwemo za LATRA na huduma za udhibiti wa usafiri ardhini bila kuchoka.

Mwisho, kwa wadau wetu na Watanzania wote kwa ujumla, tunawaomba tuendeleze **umoja, mshikamano, amani, upendo, utulivu, ushirikiano, kusaidiana na kuheshimiana** na kamwe tusibaguane kwa rangi, dini, kabila, jinsia, kanda au rika. Tuzidi kumuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema na umri mrefu **Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Mhe. Rais wetu ametuongoza kwa mifano kupitia **falsafa yake ya 4R** iliyojikita katika masuala ya **Maridhiano** ***(Reconciliation),*** **Ustahamilivu** ***(Resilience),*** **Mageuzi** ***(Reforms), na*** **Kujenga upya Taifa** ***(Rebuilding).*** Tunamtakia mafanikio makubwa zaidi kwenye Uchaguzi Mkuu ujao wa mwaka huu, 2025 na tunamuomba Mungu amjaalie kuendelea kuliongoza Taifa letu na kuendeleza kasi ya maendeleo ya Nchi.

***Asanteni sana kwa kunisikiliza.***



Digitally Signed By Habibu J. S. Suluo
Mon Apr 14 09:19:02 EAT 2025

Habibu J. S. Suluo

**MKURUGENZI MKUU- LATRA**